# SERIKALI YA MAPINDUZI ZANZIBAR

## WIZARA YA ELIMU NA MAFUNZO YA AMALI

## MUHTASARI WA KISWAHILI
### KWA ELIMU YA MAANDALIZI ZANZIBAR

## TAASISI YA ELIMU ZANZIBAR

## 2012

© Wizara ya Elimu na Mafunzo ya Amali, 2012

Haki zote zimehifadhiwa, hairuhusiwi kuiga, kunakili, kutafsiri, kupiga chapa, maandishi nukta nundu na kutoa Muhtasari huu kwa jinsi yoyote ile bila ya idhini ya Wizara ya Elimu na Mafunzo ya Amali.

Umetayarishwa na:
Taasisi ya Elimu Zanzibar
S.L.P. 840
**Zanzibar**

# YALIYOMO

Ukurusa

YALIYOMO ... ii
Utangulizi ... iii
Ujuzi wa Jumla wa Somo la Kiswahili ... iii
Malengo ya Jumla ya Somo la Kiswahili ... iv
MUHTASARI WA KISWAHILI KWA MWAKA WA KWANZA ... 1
MWAKA WA PILI ... 12

## KISWAHILI

# Utangulizi

Kiswahili ni lugha mama kwa mtoto wa Kizanzibari. Wataalamu wanaamini kuwa mtoto hujifunza kwa haraka zaidi kwa kutumia lugha yake mama.

Kwa kuwa Kiswahili ndio lugha ambayo mtoto huanza kuisikia tangu anapozaliwa, hivyo huweza kufahamu kwa haraka na kuzimudu stadi mbali mbali za lugha pamoja na kujiamini na kuwa na fursa ya kuzungumza. Hivyo jambo muhimu ni kuhamasishwa na kusaidiwa namna ya kutumia stadi hizo.

Stadi hizi zinajumuisha kuzungumza, kusikiliza, kusoma na kuandika.

## Ujuzi wa Jumla wa Somo la Kiswahili

Baada ya kujifunza somo la Kiswahili katika skuli za Maandalizi, watoto wataonesha ujuzi wa:-

1. Kuzungumza na kujieleza kwa watoto wenzao walimu na watu wengine.
2. Kutumia lugha ya alama kwa viziwi na wenye ulemavu wa akili kusikiliza watoto wenzao, walimu na watu wengine ili kupata msamiati pamoja na kufuata maelekezo.
3. Kusoma vitabu vidogo kwa kuangalia picha.
4. Kusoma sentensi ndogo ndogo.
5. Kuchora picha zisizo na mnasaba na zenye mnasaba na vitu.
6. Kusoma majina yao.
7. Kusikiliza sauti zilizorikodiwa.
8. Kuelezea michoro na picha walizochora mbele ya wenzao.
9. Kutumia lugha kwa furaha kupitia nyimbo, hadithi, vitendawili na vizunguka ulimi.

## Malengo ya Jumla ya Somo la Kiswahili

Somo la Kiswahili linafundishwa katika skuli za Maandalizi ili watoto waweze:

1. Kupata stadi za kuzungumza na kujieleza kwa watoto wenzao, walimu na watu wengine kwa watoto viziwi watatumia lugha ya alama.
2. Kufurahia lugha ya Kiswahili kupitia nyimbo, hadithi, vitendawili na vizunguka ulimi.
3. Kupata stadi za kusikiliza kutoka kwa watoto wenzao, walimu na watu wengine ili kukuza msamiati, kufuata maelekezo na kukuza ufahamu.
4. Kupata stadi za usomaji wa vitabu vidogo vidogo kwa kuangalia picha pamoja na usomaji wa sentensi ndogo ndogo..
5. Kuelewa usomaji wa majina yao.
6. Kupata stadi za kusikiliza sauti zilizorikodiwa.
7. Kujenga uwezo wa uelezaji wa picha walizozichora mbele ya wenzao.
8. Kupata uzoefu wa ukuzaji wa misuli yao kwa uchoraji wa picha zisizo na zenye mnasaba na vitu

# MUHTASARI WA KISWAHILI KWA MWAKA WA KWANZA

| MADA KUU/MADA NDOGO | MALENGO MAHSUSI | MBINU ZA KUFUNDISHIA/ KUJIFUNZIA | VIFAA | VIPINDI |
|---|---|---|---|---|
| 1. KUSIKILIZA NA KUZUNGUMZA<br>(a) Kufuata Maelekezo | Mtoto aweze Kutekeleza amri ya aina moja kwa wakati mmoja. | 1. Kwa kutumia mbinu ya Igizo mwalimu awaongoze watoto kufanya kitendo kimoja kwa wakati.<br>2. Kwa kutumia mbinu ya Michezo mwalimu awaongoze watoto kutekeleza amri ya aina moja kwa wakati mmoja. | 1. Vitu vya darasani<br>2. Majuso<br>3. Firimbi<br>4. Bendera za rangi. | 2 |
| (b) Hadithi | Mtoto aweze :-<br>(i) Kujibu maswali yaliyotokana na hadithi. | Kwa kutumia mbinu ya Maswali na Majibu mwalimu awaongoze watoto kujibu maswali kutokana na hadithi waliiyosikiliza. | 1. Vitabu vya hadithi/nukta nundu<br>2. Chati ya hadithi/chati mguso<br>3. Vifaa vinavyohusu hadithi. | 6 |
| | (ii) Kuigiza matukio ya hadithi. | Kwa kutumia mbinu ya Igizo mwalimu awaongoze watoto kuigiza | 1. Vitabu vya hadithi/nukta | |

| MADA KUU/MADA NDOGO | MALENGO MAHSUSI | MBINU ZA KUFUNDISHIA/ KUJIFUNZIA | VIFAA | VIPINDI |
|---|---|---|---|---|
| | | matukio mepesi yaliyojitokeza katika hadithi. | nundu<br>2. Chati ya hadithi/chati mguso.<br>3. Majuso.<br>4. Vifaa vinavyohusu hadithi. | |
| | (iii) Kusimulia hadithi. | Kwa kutumia mbinu ya Maswali na Majibu mwalimu awaongoze watoto kusimulia hadithi waliyosomewa/kusimuliwa. | 1. Vitabu vya hadithi/nukta nundu<br>2. Majuso<br>3. Chati ya hadithi/mguso<br>4. Vikaragosi<br>5. Kanda.<br>6. | |
| (c) Nyimbo | Mtoto aweze:-<br>(i) Kusikiliza na kuimba nyimbo. | 1. Kwa kutumia mbinu ya Nyimbo mwalimu awaongoze watoto kusikiliza na kuimba nyimbo.<br>2. Kwa kutumia mbinu ya Nyimbo | 1. Kanda<br>2. Kinasa sauti<br>3. T.V.<br>4. Video | 4 |

| MADA KUU/MADA NDOGO | MALENGO MAHSUSI | MBINU ZA KUFUNDISHIA/ KUJIFUNZIA | VIFAA | VIPINDI |
|---|---|---|---|---|
| | | mwalimu awaongoze watoto kuimba. | 5. Vitabu vya nyimbo/nukta nundu. | |
| | (i) Kuigiza mnasaba na nyimbo. | 1. Kwa kutumia mbinu ya Onesho mwalimu awaongoze watoto kuigiza vitendo katika nyimbo.<br>2. Kwa kutumia mbinu ya Igizo mwalimu awaongoze watoto kuigiza. | Vifaa vya kuigiza vinavyohusu nyimbo. | |
| | (ii) Kufuata mianguko ya sauti. | Kwa kutumia mbinu ya Onesho mwalimu awaongoze watoto kuzingatia mianguko ya sauti. | Vikaragosi. | |
| (d) Vitendawwili na Vizunguka Ulimi | Mtoto aweze:-<br>(i) Kutegua Vitendawili vyepesi | Kwa kutumia mbinu ya Onesho mwalimu awaongoze watoto kutegua vitendawili vyepesi. | 1. Kanda za majibu ya vitendawili<br>2. vitendawili/kadi | 5 |
| | . | | 3. mguso<br>Vitu halisi. | |
| | (ii) Kutega vitendawili vyepesi. | 1. Kwa kutumia mbinu ya Michezo mwalimu awaongoze watoto kutega vitendawili vyepesi.<br>2. Kwa kutumia mbinu ya Picha ya | 1. Kadi za picha za majibu ya vitendawili.<br>2. Vitu halisi. | |

| MADA KUU/MADA NDOGO | MALENGO MAHSUSI | MBINU ZA KUFUNDISHIA/ KUJIFUNZIA | VIFAA | VIPINDI |
|---|---|---|---|---|
| | | Kuiga mwalimu awaongoze watoto kutega vitendawili wenyewe. | | |
| | (iii) Kutamka vizunguka ulimi vyepesi. | 1. Kwa kutumia mbinu ya Onesho mwalimu awaongoze watoto kutamka vizunguka ulimi vyepesi.<br>2. Kwa kutumia mbinu ya Kuiga mwalimu awaongoze watoto kutamka vizunguka ulimi wenyewe. | 1. Kadi za vizunguka ulimi.<br>2. Vitabu vya vizunguka ulimi/nukta nundu. | |
| (e) Kuelezea vitu. | Mtoto aweze:-<br>(i) Kutaja vitu vya darasani. | .1. Kwa kutumia mbinu ya Michezo mwalimu awaongoze watoto kutaja majina ya vitu vya darasani.<br>3. Kwa kutumia mbinu ya Nyimbo mwalimu awaongoze watoto Kutaja majina ya vitu vya darasani. | Vitu vya darasani. | 5 |
| | (ii) Kuelezea wasifu | Kwa kutumia mbinu ya Michezo | Vitu vya ndani ya | |

| MADA KUU/MADA NDOGO | MALENGO MAHSUSI | MBINU ZA KUFUNDISHIA/ KUJIFUNZIA | VIFAA | VIPINDI |
|---|---|---|---|---|
| | wa vitu. | mwalimu awaongoze watoto kuelezea wasifu wa vitu. | darasa. | |
| (a) Kuomba Samahani. | Mtoto aweze:-<br>(i) Kutumia lugha inayofaa katika kuomba msamaha. | 1. Kwa kutumia mbinu ya Igizo Mfano mwalimu awaongoze watoto kuomba msamaha.<br>2. Kwa kutumia mbinu ya Mazoezi mwalimu awaidilishe watoto kuomba msamaha. | - | 3 |
| (g) Kuonesha Shukurani. | Mtoto aweze kutumia lugha | 1. Kwa kutumia mbinu ya Igizo mfano mwalimu awaongoze | - | 3 |
| | inayofaa katika kuonesha shukurani. | watoto kutumia lugha inayofaa katika kutoa shukurani.<br>2. Kwa kutumia mbinu ya Mazoezi mwalimu awaongoze watoto kutumia lugha inayofaa katika kuonesha shukurani | - | |
| (h) Kuelezea Matukio ya Jamii. | Mtoto aweze:-<br>(i) Kuelezea matukio yaliyotokea nyumbani. | 1. Kwa kutumia mbinu ya Kisa Mafunzo mwalimu awaongoze watoto kuelezea matukio yaliyotokea nyumbani.<br>2. Kwa kutumia mbinu ya Maswali | - | 4 |

| MADA KUU/MADA NDOGO | MALENGO MAHSUSI | MBINU ZA KUFUNDISHIA/ KUJIFUNZIA | VIFAA | VIPINDI |
|---|---|---|---|---|
| | | na Majibu mwalimu awaongoze watoto kuelezea matukio yaliyotokea nyumbani. | | |
| | (ii) Kuelezea matukio yaliyotokea katika jamii. | 1. Kwa kutumia mbinu ya Mchoro Elekezi mwalimu awaongoze watoto kuelezea matukio yaliyotokea katika jamii.<br>2. . Kwa kutumia mbinu ya | Chati ya matokeo ya jamii/chati mguso. | |
| | | Maswali na Majibu mwalimu awaongoze watoto kuelezea matukio yaliyotokea katika jamii. | | |
| (i) Kujitambulisha | Mtoto aweze:-<br>(i) Kujitambulisha jina na jinsi yake. | Kwa kutumia mbinu ya Nyimbo mwalimu awaongoze watoto kila mmoja kujitambulisha mwenyewe jina na jinsi yake. | Kadi za majina/nukta nundu. | 4 |
| | (ii) Kuwatambulisha wengine. | Kwa kutumia mbinu ya Michezo mwalimu awaongoze watoto kuwatambulisha watoto wenzake. | Kadi za majina/nukta nundu. | |
| 2. KUSOMA<br>(a) Hadithi | Mtoto aweze:-<br>(i) Kusoma picha za hadithi. | Kwa kutumia mbinu ya Mchoro Elekezi mwalimu awaongoze watoto kusoma picha zinazosimulia hadithi. | Vibango vya picha za hadithi/bango mguso. | 25 |

| MADA KUU/MADA NDOGO | MALENGO MAHSUSI | MBINU ZA KUFUNDISHIA/ KUJIFUNZIA | VIFAA | VIPINDI |
|---|---|---|---|---|
| | (ii) Kujibu maswali yanayotokana katika hadithi aliyosikiliza. | Kwa kutumia mbinu ya Maswali na Majibu mwalimu awaongoze watoto kujibu maswali yanayotokana na hadithi aliyoskiliza. | Kitabu cha hadithi fupi/ nukta nundu. | |
| | (iii) Kusimulia hadithi fupi fupi. | Kwa kutumia mbinu ya Onesho mwalimu awaongoze watoto kusimulia hadithi fupi. | 1. Vitabu vya hadithi/ nukta nundu<br>2. kadi za picha za wahusika wa hadithi/ mguso. | |
| | (iv) Kuigiza hadithi fupi fupi. | Kwa kutumia mbinu ya Igizo mwalimu awaongoze watoto kuigiza hadithi fupi fupi. | 1. Vitabu vya hadithi/nukta nundu<br>2. Vifaa vya kuigiza. | |
| (b) Majina | (i) Kusoma majina Yao. | 1. Kwa kutumia mbinu ya Onesho mwalimu awaongoze watoto kusoma majina yao.<br>2. Kwa kutumia mbinu ya Michezo mwalimu awaongoze watoto kusoma majina yao. | Kadi za majina/nukta nundu. | 8 |

| MADA KUU/MADA NDOGO | MALENGO MAHSUSI | MBINU ZA KUFUNDISHIA/ KUJIFUNZIA | VIFAA | VIPINDI |
|---|---|---|---|---|
| | (ii) Kusoma majina ya vitu kwa picha. | Kwa kutumia mbinu ya Onesho mwalimu awaongoze watoto kusoma picha kuelezea hadithi inayotokana na picha. | 1. Vibango vya picha/ mguso.<br>2. Jig saw puzzle. | |
| (c) Herufi | Mtoto aweze kusoma herufi za alfabeti. | 1. Kwa kutumia mbinu ya Nyimbo mwalimu awaongoze watoto kusoma herufi za alfabeti.<br>2. Kwa kutumia mbinu ya Michezo mwalimu awaongoze watoto kusoma herufi za alfabeti.<br>3. Kwa kutumia mbinu ya Kumechisha mwalimu awaongoze watoto kusoma herufi za alfabeti. | 1. Chati la alfabeti/ Chati ya lugha ya alama<br>2. Kadi za herufi moja moja/nukta nundu<br>3. Kadi za alfabeti/nukta nundu. | 5 |
| (d) Maneno | Mtoto aweze kusoma maneno. | 1. Kwa kutumia mbinu ya Kumechisha neno kwa picha mwalimu awaongoze watoto kusoma maneno. | 1. Kadi za picha za wahusika kutokana na hadithi/nukta | 5 |
| | | 2. Kwa kutumia mbinu ya Kumechisha neno kwa neno mwalimu awaongoze watoto | nundu.<br>2. Kadi za majina ya wahusika/chati | |

| MADA KUU/MADA NDOGO | MALENGO MAHSUSI | MBINU ZA KUFUNDISHIA/ KUJIFUNZIA | VIFAA | VIPINDI |
|---|---|---|---|---|
| | | kusoma maneno.<br>3. Kwa kutumia mbinu ya Michezo mwalimu awaongoze watoto kusoma maneno. | mguso<br>3. "Jig - saw puzzle chati mguso. | |
| (d) Silabi | Mtoto aweze kusoma silabi. | 1. Kwa kutumia Onesho Mbinu mwalimu awaongoze watoto kusoma silabi.<br>2. Kwa kutumia mbinu ya Michezo mwalimu awaongoze watoto kusoma silabi. | 1. Kadi za silabi/nukta nundu<br>2. Kadi za majina ya wahusika kutokana na hadithi/nukta nundu mguso<br>3. Puzzles. | 6 |
| 3. KUANDIKA<br>(a) Kuchora na Kupaka Rangi. | Mtoto aweze:-<br>(i) Kupaka rangi picha. | Kwa kutumia mbinu ya Onesho mwalimu awaongoze watoto kupaka rangi picha alizochorewa. | 1. Karatasi, Penseli.<br>2. Krayons.<br>3. Rangi za maji<br>4. Vibao (sleti). | 6 |
| | (ii) Kuchora na kupaka rangi picha. | Kwa kutumia mbinu ya Nyimbo mwalimu awaongoze watoto kuchora picha zao wenyewe na | 1. Karatasi<br>2. Penseli za rangi<br>3. Mabuku | |

| MADA KUU/MADA NDOGO | MALENGO MAHSUSI | MBINU ZA KUFUNDISHIA/ KUJIFUNZIA | VIFAA | VIPINDI |
|---|---|---|---|---|
| | | kuzipaka rangi. | 4. Vibao. | |
| (b) Nakshi za Msingi | Mtoto aweze kuandika/kuchora nakshi za msingi. | 1. Kwa kutumia mbinu ya Nyimbo mwalimu awaongoze watoto kuandika/kuchora nakshi nane za msingi.<br>2. Kwa kutumia mbinu ya Igizo Mfano mwalimu awaongoze watoto kuchora nakshi nane za msingi.<br>3. Kwa kutumia mbinu ya Mazoezi ya Kurudia rudia mwalimu awaongoze watoto kuandika/kuchora nakshi za msingi. | 1. Chati za nakshi za msingi/ mguso<br>2. Penseli<br>3. Penseli za rangi.<br>4. Krayons sleti<br>5. Karatasi. | 16 |
| (c) Herufi | Mtoto aweze kuandika herufi za alfabeti ya Kiswahili. | 1. Kwa kutumia mbinu ya Onesho mwalimu awaongoze watoto kuandika herufi za alfabeti za msingi kutokana na nakshi za msingi<br>2. Kwa kutumia mbinu ya Kupaka Rangi mwalimu awaongoze | 1. Penseli<br>2. Karatasi<br>3. Buku<br>4. Rangi<br>5. Krayons<br>6. Madaftari ya kuandikia | 6 |

| MADA KUU/MADA NDOGO | MALENGO MAHSUSI | MBINU ZA KUFUNDISHIA/ KUJIFUNZIA | VIFAA | VIPINDI |
|---|---|---|---|---|
| | | watoto kuandika herufi za alfabeti ya Kiswahili | 7. Sleti. | |
| (d) Silabi | Mtoto aweze kuandika silabi za muundo sahili. | Kwa kutumia mbinu ya Onesho mwalimu awaongoze watoto kuandika silabi za muundo wa konsonanti moja na irabu moja. | 1. Penseli<br>2. Madaftari ya kuandikia. | 5 |
| (e) Maneno | Mtoto aweze Kuandika jina lake na maneno ya silabi mbili. | Kwa kutumia mbinu ya Onesho mwalimu awaongoze watoto kuandika majina yao na maneno ya silabi mbili. | 1. Kadi za silabi/nukta nundu<br>2. Kadi za maneno/ nukta nundu<br>3. Penseli<br>4. Karatasi<br>5. Madaftari. | 5 |

# MWAKA WA PILI

| MADA KUU/MADA NDOGO | MALENGO MAHSUSI | MBINU ZA KUFUNDISHIA/ KUJIFUNZIA | VIFAA | VIPINDI |
|---|---|---|---|---|
| 1. KUSIKILIZA NA KUZUNGUMZA<br>(a) Kufuata Maelekezo | Mtoto aweze Kutekeleza amri zaidi ya moja kwa wakati mmoja. | Kwa kutumia mbinu ya Igizo mwalimu awaongoze watoto kutekeleza amri zaidi ya moja kwa wakati mmoja. | Vifaa vya darasani au bila ya vifaa. | 2 |
| (b) Hadithi | Mtoto aweze:-<br>(i) Kujibu maswali yanayotokana na hadithi kwa kujenga hoja. | Kwa kutumia mbinu ya Maswali na Majibu mwalimu awaongoze watoto kujibu maswali kwa kutumia hoja kutokana na hadithi waliyoisikiliza. | 1. Vitabu vya hadithi/nukta nundu<br>2. Sinema (filamu) | 2 |
| | (ii) Kutabiri kinachofuata katika hadithi inayosimuliwa. | Kwa kutumia mbinu ya Kutabiri mwalimu awaongoze watoto kutabiri kinachofuata katika hadithi inayosimuliwa. | 1. Vitabu vya hadithi/nukta nundu<br>2. Sinema (filamu)<br>3. Bango la fulana<br>4. Kadi za picha/mguso. | |
| | (iii) Kuchangia | 1. Kwa kutumia mbinu ya Onesho | 1. Karatasi. | |

| MADA KUU/MADA NDOGO | MALENGO MAHSUSI | MBINU ZA KUFUNDISHIA/ KUJIFUNZIA | VIFAA | VIPINDI |
|---|---|---|---|---|
| | mtiririko wa matukio katika kubuni hadithi. | mwalimu awaongoze watoto kusimulia hadithi kwa kuchangia mtiririko wa matukio katika kubuni hadithi.<br>2. Kwa kutumia mbinu ya Mchoro mwalimu awaongoze watoto kuchora picha kuonesha mtiririko wa matukio katika kubuni hadithi. | 2. Madaftari ya kuandikia<br>3. Krayons<br>4. Penseli. | |
| | (iv) Kusimulia hadithi fupi. | 1. Kwa kutumia mbinu Onesho mwalimu awaongoze watoto kusimulia hadithi fupi kwa kuzingatia kanuni za usimuliaji.<br>2 Kwa kutumia mbinu ya Igizo mwalimu awaongoze watoto kuigiza hadithi fupi iliyosimuliwa. | 1. Vitabu vya hadithi<br>2. Simena<br>3. Bango la fulana. | |
| (c) Nyimbo | Mtoto aweze kufuata mianguko ya sauti. | Kwa kutumia mbinu ya Kuiga mwalimu awaongoze watoto kufuata mianguko ya sauti. | Vitabu vya nyimbo/nukta nundu. | 2 |
| (d) Vitendawili na | Mtoto aweze: | 1. Kwa kutumia mbinu ya Mashairi | Vitabu/Vitabu katika | 6 |

| MADA KUU/MADA NDOGO | MALENGO MAHSUSI | MBINU ZA KUFUNDISHIA/ KUJIFUNZIA | VIFAA | VIPINDI |
|---|---|---|---|---|
| Vizunguka Ulimi | (i) Kutega na kutegua vitendawili. | mwalimu awaongoze watoto kutega na kutegua vitendawili vya mashairi.<br>2. Kwa kutumia mbinu ya Kuiga mwalimu awaongoze watoto kutega na kutegua vitendawili wenyewe. | nukta nundu. | |
| | (ii) Kutamka vizunguka ulimi vigumu. | Kwa kutumia mbinu ya Kuiga mwalimu awaongoze watoto kutamka vizunguka ulimi vigumu. | Vitabu/Vitabu katika nukta nundu. | |
| (e) Kuomba Ruhusa | Mtoto aweze Kutumia lugha inayofaa wakati wa kuomba ruhusa. | Kwa kutumia mbinu ya Igizo mwalimu awaongoze watoto kutumia lugha inayofaa wakati wa kuomba ruhusa. | - | 2 |
| (f) Kueleza Matukio ya Jamii. | Mtoto aweze:-<br>(i) Kueleza tukio alililoliona njiani. | Kwa kutumia mbinu ya kisa mafunzo mwalimu awaongoze watoto kueleza matukio waliyoyaona njiani. | - | 4 |
| | (ii) Kuelezea tukio lililotokea katika | Kwa kutumia mbinu ya Kisa Maelezo mwalimu awaongoze watoto | - | |

| MADA KUU/MADA NDOGO | MALENGO MAHSUSI | MBINU ZA KUFUNDISHIA/ KUJIFUNZIA | VIFAA | VIPINDI |
|---|---|---|---|---|
| | jamii. | kuelezea matukio yaliyojitokea katika jamii. | | |
| 2. KUSOMA<br>(a) Hadithi | Mtoto aweze<br>(i) Kusoma picha. | Kwa kutumia mbinu ya Maswali na Majibu mwalimu awaongoze watoto kusoma picha kutokana na hadithi. | 1. Kitabu cha hadithi./kitabu katika nukta nundu<br>2. Sinema (filamu)<br>3. Puppet/ karagosi<br>4. Picha/chati mguso.<br>5. Picha kutokana na hadithi. | 8 |

| MADA KUU/MADA NDOGO | MALENGO MAHSUSI | MBINU ZA KUFUNDISHIA/ KUJIFUNZIA | VIFAA | VIPINDI |
|---|---|---|---|---|
| | (ii) Kusoma majina. | 1. Kwa kutumia mbinu ya Mashindano mwalimu awaongoze watoto kusoma majina ya wahusika wa hadithi.<br>2. Kwa kutumia mbinu ya Kumechisha mwalimu awaongoze watoto kusoma majina ya wahusika kutokana na hadithi.<br>1. Kwa kutumia mbinu ya Michezo mwalimu awaongoze watoto kusoma majina ya wahusika kutokana na hadithi. | 2. Karagosi<br>3. kadi za majina ya watoto<br>3. Bango la fulana<br>4. Kadi za majina ya mahusika.<br>5. Chati/Chati mguso. | |

| MADA KUU/MADA NDOGO | MALENGO MAHSUSI | MBINU ZA KUFUNDISHIA/ KUJIFUNZIA | VIFAA | VIPINDI |
|---|---|---|---|---|
| (b) Maneno | Mtoto aweze Kusoma maneno yenye silabi mbili au tatu. | 1. Kwa kutumia mbinu ya onesho mwalimu awaongoze watoto kusoma maneno ya silabi mbili au tatu.<br>2. Kwa kutumia mbinu ya Mazoezi mwalimu awaongoze watoto kuunda na kusoma maneno yenye silabi mbili au tatu. | - | 15 |
| (c) Kusoma silabi | Mtoto aweze kusoma silabi. | Kwa kutumia mbinu ya Onesho mwalimu awaongoze watoto kusoma silabi kutokana na majina ya wahusika wa hadithi. | 1. Skittles<br>2. Bango la fulana<br>3. kadi za silabi/Kadi katika nukta nundu. | 14 |
| (d) Sentensi | Mtoto aweze<br>(i) Kupanga sentensi fupi. | Kwa kutumia mbinu ya Michezo mwalimu awaongoze watoto kupanga maneno ili kupata sentensi fupi na kuzisoma. | 1 Kadi za maneno/kadi katika nukta nundu. | 8 |
| | (ii) Kusoma sentensi | Kwa kutumia mbinu ya Mazoezi | 1. Kitabu cha | |

| MADA KUU/MADA NDOGO | MALENGO MAHSUSI | MBINU ZA KUFUNDISHIA/ KUJIFUNZIA | VIFAA | VIPINDI |
|---|---|---|---|---|
| | fupi. | mwalimu awaongoze watoto kusoma sentensi fupi. | hadithi/kitabu katika nukta nundu<br>2. kadi ya sentensi./kadi katika nukta nundu<br>3. Chati/chati mguso. | |
| (e) Vitabu | Mtoto aweze kusoma vitabu vyenye maneno machache. | Kwa kutumia mbinu ya Kusaidiana wenyewe kwa wenyewe mwalimu awaongoze watoto kusoma hadithi zenye maneno machache. | Vitabu vya kutengenezwa na mwalimu na watoto. | 8 |
| 3. KUANDIKA<br>(a) Kuchora na Kupaka Rangi | Mtoto aweze Kuchora na kupaka rangi picha zake za kubuni. | Kwa kutumia mbinu ya Mazoezi mwalimu awape fursa watoto kuchora na kupaka rangi picha zao za kubuni. | 1. Penseli.<br>2. Daftari la kuandikia.<br>3. Karatasi.<br>4. Karagosi/penseli za rangi. | 5 |

| MADA KUU/MADA NDOGO | MALENGO MAHSUSI | MBINU ZA KUFUNDISHIA/ KUJIFUNZIA | VIFAA | VIPINDI |
|---|---|---|---|---|
| (b) Silabi | Mtoto aweze kuandika silabi. | Kwa kutumia mbinu Onesho mwalimu awaongoze watoto kuandika silabi. | 1. Kadi za silabi.<br>2. Daftari la kuandikia<br>3. Karatasi za fotokopi. | 15 |
| (c) Maneno | Mtoto aweze Kuandika maneno. | Kwa kutumia mbinu ya Onesho mwalimu awaongoze watoto kuandika maneno. | 1 Kadi za Maneno/kadi katika nukta nundu<br>2. Karatasi<br>3. Madaftari ya kuandikia<br>4. Karatasi za fotokopi. | 10 |
| (d) Sentensi | Mtoto aweze kunakili sentensi. | Kwa kutumia Onesho Mbinu mwalimu awaongoze watoto kunakili sentensi fupi kwa kunakili. | 1. Kadi za sentensi<br>2. Karatasi | 10 |